



# COVID-19

## JINSI YA KUPATA CHANJO YAKO

Hakikisha kuwa unapata chanjo yako unapokuwa unastahiki ili uweze kulindwa. Ikiwa huwezi kufanya mchakato huu mtandaoni, wasiliana na Nambari ya Msaada ya Chanjo ya Nevada, 1.800.401.0946. Ikiwa unajua kompyuta na unamjua mtu anayeweza kupata changamoto kwenye mchakato huu, tafadhali mpatie usaidizi wako.

### HATUA YA 1: TAFUTA ENEO LA CHANJO

- Maeneo yote ya chanjo kwenye kaunti yako yanaweza kupatikana kwenye [nvcovidfighter.org](https://nvcovidfighter.org), ukurasa wa Kaunti Maalum, au kwa kuipigia simu Nambari ya Msaada ya Chanjo ya Nevada, 1.800.401.0946, 8 AM hadi 8 PM, siku 7 kwa wiki (Wazungumzaji wa lugha kadhaa wanapatikana mtandaoni).



### HATUA YA 2: SAJILI KWENYE TOVUTI

- Pindi unapotambua eneo, zuru tovuti ya eneo hilo ili kupanga miadi yako.
- Kwa wale wenye umri wa miaka 16-17, thibitisha kuwa eneo linatoa chanjo ya Pfizer, chanjo pekee iliyoidhinishwa kwa 16+ (Kwa wakati huu, hakuna chanjo zilizoidhinishwa kwa wale wenye umri wa chini ya miaka 16).
- Huenda ukahitaji kuunda wasifu wa mtumiaji na kujibu maswali kuhusu ustahiki wako.



### HATUA YA 3: CHAGUA WAKATI/TAREHE YA MIADI

- Pindi unaposajiliwa, tafuta miadi inayopatikana.
- Huenda ikabidi ujaribu kwa kujirudia kwenye maeneo anuwai.
- Kuwa na subira. Kwa ajili ya maongezeko ya hivi karibuni ya uzalishaji chanjo, karibuni kutakuwa na miadi huria na ufikishaji zaidi.

### HATUA YA 4: JITAYARISHE KWA MIADI YAKO

- Ikiwa kuna fomu, zikamilishe kabla ya miadi au wasili mapema ili kuzikamilisha.
- Ikiwa huwezi kufika kwenye miadi yako, tafadhali ghairi.

### HATUA YA 5: LETA KITAMBULISHO/ UTHIBITISHAJI

- Itabidi uonyeshe kitambulisho.
- Faragha yako inalindwa.
- Maelezo yako ya kibinafsi yanashirikiwa na serikali ya shirikisho.

### HATUA YA 6: RATIBU DOZI YA 2 (IKIWA INAHUSISHWA)

- Ratibu dozi yako ya 2 ikiwa unapokea chanjo ya Pfizer au Moderna.
- Ili kupata kumbusho la dozi ya 2, jiandikishe kwenye VaxText kwa kutuma ujumbe wa **ENROLL** kwa **1.833.829.8398**.
- Ili kuarifu CDC kuhusu athari zozote mbadala, **jiandikishe kwenye [vsafe.cdc.gov](https://vsafe.cdc.gov)**.



### HATUA YA 7: PATA DOZI YA 2 (IKIWA INAHUSISHWA)

- Ikiwa ulipokea chanjo ya Pfizer au Moderna, hakikisha kuwa unapata dozi yako ya 2 kwenye tarehe iliyoratibiwa ili kulindwa kikamilifu.
- Ukipokea chanjo ya Janssen, unachanjwa kikamilifu baada ya dozi moja.

**Tafuta eneo la chanjo**  
**[nvcovidfighter.org](https://nvcovidfighter.org) | 1.800.401.0946**

